

FOMU YA MKATABA WA UJENZI

A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

| | | |
|---|---|--|
| 1 | MWAJIRI | Mkuu wa Chuo VETA Dodoma S. L. P. Dodoma - Tanzania |
| 2 | JINA NA ANWANI YA FUNDI (Mwajiriwa) | Jina: ELIUD EPHRAIMU KAMWELA Anwani: S. L. P. 2197 Simu: 0744-759640 Account number: 51710043525 |
| 3 | ENEO LA UJENZI | BAHI -DVTC |
| 4 | MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI | Kupiga plastia milango (4) na kunyoasha kopo/bwalo la Chakula, Kupiga plastia milango (1) kwenye nyumba ya mkuu wa Chuo |
| 5 | GHARAMA YA UFUNDI | TSHS 120,000/= |
| 6 | MUDA WA MKATABA (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba): | Tarehe ya Kusainiwa 21-04-2022 Muda: (Siku) Tarehe ya Kuanza Kazi 20-04-2022 Tarehe ya Kumaliza Kazi 22-04-2022 |
| 7 | MASHARTI YA MALIPO: | <ul style="list-style-type: none"> • Hakuna Malipo ya Awali • Fundi atalipwa kwa awamu baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa |

B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama "concrete mixer", toroli, karai, ndoo, chepe, ngazi, n.k.
3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asijiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
7. Fundi atahusika na vitendo (*kama wizi, uharibifu wa mali za chuo*) vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika (*Retention Money*) na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
10. Ucheleweshaji wa Kazi:
 - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

11. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwijiri (kutokana na fedha au vifaa), Fundi ataongezewa muda wa kumaliza kazi.

12. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.

MWAJIRI:

Saini: 

Jina: STIBARA

Cheo: AG. PRINCIPAL

Tarehe:

FUNDI/KIBARUA

Saini: E. Ephraimu

Jina: ELIUD EPHRAIMU KAMWELD

Cheo: FUNDI MKUU

Tarehe: 22 04 - 2022

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini: 

Jina: RAMADHANI IBRAHIM NKANI

Cheo: SITE ENGINEER

Tarehe: 21/04/2022

SHAHIDI WA FUNDI/KIBARUA

Saini: E. Kusenha

Jina: EMMANUEL KUSENHA

Cheo: FUNDI

Tarehe: 22/04/2022